

**MAOMBI**

**YENYE**

**MAJIBU**

## **Hakimiliki**

**© Nabii Mkuu Pd Yohana**

Hakizote zimehifadhiwa.

Kamwe hairuhusiwikunakili, kuweka kwenye mtandao, kubadirisha, kutafasiri katika lugha yeyote ile au kuchapisha upya chapisho hili bila idhini ya mwandishi.

Nabii Mkuu Pd Yohana

S.L.P 4016

Mwanza Tanzania

Simu : +255 762 415790, +255 759 204 744

[Yohanayona3@gmail.com](mailto:Yohanayona3@gmail.com)

[www.hlcenter.info](http://www.hlcenter.info)

ISBN : -----

Toleo la Kwanza 2025.

Kupigwa chapa na

Josia Pd John

Dar es salaam Tanzania

Simu: +255 758 588 127, +255 693 522 834

[Josiajohn735@gmail.com](mailto:Josiajohn735@gmail.com)

## **Ushuhuda Wangu Kuhusu Maombi**

*Baada ya kumpokea Yesu Kristo kama  
Bwana na Mwokozi wa maisha yangu,  
nilianza safari ya maombi iliyojaa ushindi  
na furaha isiyoweza kuelezeaka. Mwanzoni,  
kila nilipoomba, Mungu alijibu mara moja,  
na hali hii ilinipa nguvu ya kiroho na  
kujiona nikiwa karibu sana na Mungu.*

*Hata hivyo, baada ya muda, nilianza  
kupitia mabadiliko yasiyoeleweka. Nilihisi  
kama Mungu ameacha kunisikiliza, na  
hakuna maombi yangu yaliyojibiwa tena  
kama awali. Nilipokuwa nikiomba,  
kulikuwa na kimya cha ajabu. Moyo wangu  
ulianza kuhisi maumivu, na nikaanza  
kujiuliza maswali magumu kama, "Je,  
Mungu ameniacha?" au "Je, hanipendi tena  
kama hapo awali?"*

*Hali hii ilizidi kuwa ngumu, na nikajikuta nikipoteza matumaini katika wokovu. Nilianza kukata tamaa kwa kiwango cha kufikiria kuacha kumtumikia Mungu kabisa. Nilijawa na mawazo ya kukata tamaa kiasi kwamba hata nilifikiria kujiua. Hali yangu ilikuwa mbaya sana, na nilihitaji msaada wa kiroho kwa haraka.*

*Katika hali hiyo ya giza, Mungu hakuacha kunitazama. Siku moja nilihudhuria ibada ambapo mhubiri alihubiri juu ya Maombi Yenye Majibu. Ujumbe huu ulikuwa baraka ya kipekee maishani mwangu, kwani ulinijia kama mwanga katika giza nene. Kwa mara ya kwanza, nilielewa kuwa majibu ya Mungu hayaji kwa njia moja tu. Mungu anaweza kusema "ndiyo," "hapana," au "subiri."*

*Ufahamu huu ulileta mabadiliko makubwa ndani yangu. Nilianza kuelewa kuwa hata wakati Mungu yupo kimya, hajaniacha. Badala yake, yupo kazini kunifundisha uvumilivu, imani, na kutegemea mapenzi*

*yake. Furaha ya wokovu ilirejea, na moyo wangu ulianza kujaa tumaini jipya.*

*Ingawa wakati huo nilikuwa sina makazi na niliishi milimani, hali hiyo sikuiangalia tena kama adhabu. Badala yake, niliiona kama sehemu ya mpango wa Mungu wa kuniimarisha kiroho. Nilijifunza kuwa Mungu huwa hachelewi wala hawahi; Yeye hujibu maombi yetu kwa wakati wake kamili na kwa namna inayofaa zaidi kwetu.*

*Matumaini haya mapya yaliniimarisha zaidi kiroho na kunipa nguvu ya kuendelea kumtumikia Mungu kwa ujasiri. Nikaanza kuona kila hali niliyokutana nayo kama fursa ya kumshukuru Munqu na kumtumainia zaidi. Nilijifunza kwamba safari ya maombi ni ya uvumilivu, imani, na kujiweka chini ya mapenzi ya Mungu.*

*Kitabu hiki, Maombi Yenye Majibu, ni matokeo ya safari yangu ya maombi ya zaidi ya miaka 16 ya kumtumikia Mungu. Ni ushuhuda wa jinsi Mungu alivyo*

*mwaminifu, jinsi alivyonyivusha nyakati  
ngumu, na jinsi maombi yanavyoweza  
kubadilisha maisha yetu tukimtumainia  
Yeye kwa moyo wote. Naamini ushuhuda  
huu na mafundisho ndani ya kitabu hiki  
yatakuwa msaada mkubwa kwa kila mtu  
anayesaka majibu kutoka kwa Mungu.*